JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram"**AFYA**", **DODOMA**
NambariyaSimu: **+255 026 – 2323267**
E- Mail Na. ps@afya.go.tz

MjiwaSerikaliMtumba,
BarabarayaAfya,

**40478 DODOMA.**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

**Dar es Salaam, Jumatatu, Aprili 20, 2020**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatoa taarifa kuwa sampuli zilizopimwa katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii kati ya tarehe 18 hadi 20 Aprili, 2020 zimethibisha kuwepo kwa wagonjwa wapya **84** wenye maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) nchini. Kati ya hawa wagonjwa 16 ni waliotolewa Taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar leo tarehe 20 April 2020.

Kwa upande wa Tanzania bara Idadi ya wagonjwa na mikoa wanayotoka kwenye mabano ni kama ifuatavyo; Dar es Salaam (33), Arusha (4), Mbeya (3), Kilimanjaro (3), Pwani (3), Tanga (3), Manyara (2), Tabora(1), Dodoma (3), Ruvuma (2), Morogoro (2),Lindi (1), Mara (1), Mwanza (3),Mtwara (1),Kagera (1), Rukwa (2).

Wagonjwa wote walioripotiwa Tanzania Bara wanaendelea vizuri isipokuwa wagonjwa wane wanaopatiwa huduma za wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum.

Aidha, tarehe 18 April 2020, Waziri wa Afya wa Zanzibar alitoa Taarifa ya uwepo wa wagonjwa **23**. Ongezeko la wagonjwa wapya linafanya idadi ya watu waliopata maambukizi ya ugonjwa wa Corona nchini kufikia **254** kutoka wagonjwa **147** tuliowatolewa Taarifa tarehe 17 April 2020.

Aidha, tunasikitika kutangaza vifo vitatu (**3**) vilivyotokea jijini Dar es Salaam vya watu waliothibitishwa kuwa na maambukizi ya COVID-19. Wizara inatoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa marehemu.

**Ummy Mwalimu**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**